## D. Sarufi

### Usemi halisi na usemi wa taarifa

Shirikianeni kutambua sentensi za usemi halisi na za usemi wa taarifa katika orodha hii ya sentensi.

1. “Nina imani nitampata kwake leo,” shangazi alimwambia mjomba.

2. “Salome anajiheshimu na kuwaheshimu wengine kila wakati,” Kamau alisema.

3. “Utaniruhusu nikusafishie vyombo kesho?” Nora alimwuliza mama yake.

4. Shangazi alimwambia mjomba kwamba alikuwa na imani angempata kwake siku hiyo.

5. Kamau alisema kwamba Salome alijiheshimu na kuwaheshimu wengine wakati wote.

6. Nora alimwuliza mama yake kama angemruhusu amsafishie vyombo siku iliyofuata.

7. “Mwalimu alitufunza kuhusu umuhimu wa kuwa na maadili ya mtu binfsi,” Jeni alimwambia Susa.

8. Mwalimu alitufunza kuhusu umuhimu wa kuwa na maadili ya mtu binafsi.

9. Petero alimwambia Viki kwamba haikuwa vizuri kuogelea mtoni wakati huo.

10. “Hassani atamletea gilasi ya maji,” Tito alimwambia Kome.

11. Tunu alisema kwamba alikuwa amepiga deki chumba chake jioni hiyo.

12. “Mnastahili kuwatunza wanyama kila wakati,” afisa wa mifugo aliwaambia wakulima.

13. Mvuvi alisema kwamba kama angewavua samaki wengi angewagawia wenzake.

14. Ali alisema kwamba aliuziba mfereji huo siku iliyotangulia alipoupata ukitiririsha maji.